

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO



TAARIFA KWA UMMA

**SERIKALI KUTEKELEZA MIRADI KWA KUSHIRIKIANA NA SEKTA BINAFSI
YENYE THAMANI YA MABILIONI YA SHILINGI**

Serikali ya Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuanzisha na kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kwa ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) ambapo miradi zaidi ya 11 iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji lengo likiwa ni kufanikisha azma ya kuwa na uchumi wa viwanda.

Hayo yamesemwa na Kamishna wa Idara ya Ubia Sekta ya Umma na Binafsi (PPP), Wizara ya Fedha na Mipango, Dkt. John Mboya wakati akiwasilisha mada ya utekelezaji wa dhana ya ushirikishwaji wa sekta binafsi katika miradi ya maendeleo nchini kwenye semina iliyowashirikisha mawaziri, naibu mawaziri na baadhi ya watendaji wa serikali iliyofanyika kwenye ukumbi wa Wizara ya Fedha na Mipango jijini Dodoma.

Akiwasilisha mada hiyo, Dkt. John Mboya amesisitiza umuhimu wa kuwepo kwa umakini mkubwa katika uandaaji na utekelezaji wa dhana hiyo ya ubia Sekta ya Umma na Binafsi kwa kuzingatia sheria, sera, miongozo, kanuni na taratibu mbalimbali zilizopo.

Aidha alizitaka taasisi na wadau wa utekelezaji kuwa tayari kujifunza kutoka katika nchi zilizoendelea kupitia dhana hii ya ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kuchochea ukuaji wa viwanda na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Dkt. Mboya aliitaja baadhi ya miradi iliyoko katika hatua mbalimbali ya utekelezwaji kwa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi kuwa ni mradi wa mabasi yaendayo haraka (DART), Ujenzi wa Viwanda vya dawa, mradi wa VETA utakaohusisha ujenzi wa vyuo 10 ambavyo vinatarajiwa kutoa ujuzi mbalimbali kwa wanafunzi wapatao 90,000 ili kukidhi mahitaji ya wataalamu watakao saidia kufanikisha uchumi wa viwanda.

"Miradi Mingine ni Ujenzi wa Bandari ya Mwambani, barabara ya Dar es salaam hadi Chalinze, Ujenzi wa Reli kwenye miradi ya Mchuchuma hadi Mbambabay mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara, Ujenzi wa Reli kuanzia Tanga, Arusha hadi Musoma, na mradi wa umeme wa Chuo Kikuu cha Dodoma.

Akijibu swali la Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Joseph Kakunda, aliyetaka kujua kuhusu kuondolewa kwa sheria ya utekelezaji wa miradi kwa Ushirikishwaji wa Pamoja kati ya serikali na sekta binafsi (Joint Venture) ambayo haikufanikiwa kama ilivyokusudiwa hapo awali, Dkt. Mboya alisema kuwa sheria hiyo haijaondolewa bali miradi hiyo itatekelezwa kupitia sheria ya Kampuni.

Akichangia katika mjadala wa semina hiyo, Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mhandisi Stella Manyanya, alisema ni vema wakati wa kuchagua miradi wahusika wawe makini ili kuepuka kuanzisha miradi inayofanana na ambayo inaweza kuwa chanzo cha kufa kwa miradi iliyotangulia.

"Ninashauri kuwepo kwa fursa ya ushirikishwaji katika miradi midogo ambayo ina manufaa kwa wananchi ikiwemo ya ujenzi wa nyumba za waalimu" Alisema Mhandisi Manyanya

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alizitaka taasisi ambazo zinatekeleza miradi kwa ubia na sekta binafsi zielezee umma wa watanzania mafanikio yaliyopatikana ili kuhamasisha wadau wengine kufuata nyayo hizo huku akitolea mfano Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) ambalo nalo liko katika utekelezaji wa dhana hiyo.

Mwenyekiti wa semina hiyo Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Ashatu Kijaji, alisema kuwa Serikali imepeleka Muswada Bungeni unaohusu PPP, ambao ukipitishwa na Bunge linalotarajiwa kuanza Septemba 4, 2018, utekelezaji wa ubia huo utakwenda kwa kasi zaidi ili kuiwezesha nchi kufikia malengo yake ya kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya wananchi.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu, Jenister Mhagama, akiahirisha mafunzo hayo, aliwataka wadau wa semina hiyo kuendelea kukutana na kuelimishana hadi hapo marekebisho ya sheria hiyo ya Ubia Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) yatakapofanyika.

"Utekelezaji wa dhana hii ya Ubia Sekta ya Umma na Binafsi ndio njia rahisi itakayosaidia kukamilisha miradi mingi ambayo imeainishwa katika ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapainduzi (CCM) na kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, bila ushirikiano huu na sekta binafsi hatuwezi kufikia uchumi wa viwanda kwa kasi inayotakiwa" Alisema Waziri Mhagama.

Semina hiyo ya siku moja imeendeshwa na wataalamu wa masuala ya Ubia Sekta ya Umma na Binafsi kutoka Benki ya Dunia, ambapo Jumapili, kamati tatu za Bunge zitapatiwa elimu na kujengewa uwezo kuhusu dhana hiyo ya PPP.

Imetolewa na;

Benny Mwaipaja
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Wizara ya Fedha na Mipango